



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KUTOLEWA KWA MATOKEO YA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI ULIOFANYIKA
TAREHE 07.09.2023.

Dodoma – Tanzania.

02.01.2024,

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) linatangaza Matokeo ya Mtihani wa Usajili na Leseni uliyofanyika tarehe **07.09.2023** Matokeo hayo yanapatikana kwenye akaunti ya kila Mtahiniwa kwenye mfumo wa Baraza ([hppts://ww.tnmcis.go.tz](https://www.tnmcis.go.tz)).

Matokeo haya yamechelewa kutangazwa kutokana na baadhi ya watahiniwa kukiuka taratibu za ufanyaji Mitihani ambazo zimesababisha kufanyika uchunguzi ili kubaini chanzo cha ukiukwaji huo.

Baraza kwa kushirikiana na Vyombo vya Usalama limekamilisha uchunguzi na kufikia maamuzi yafuatayo: -

- i. Kutoa Matokeo ya Mtihani kwa ngazi ya Shahada (Degree) na Astashahada (Certificate) kwa kuwa hakuna Ushahidi wa ukiukwaji wa taratibu za Mtihani.
- ii. Kufuta matokeo ya Mtihani wa ngazi ya Stashahada (Diploma) baada ya kubaini ukiukwaji wa taratibu za Mtihani.
- iii. Watahiniwa wote waliofutiwa matokeo ya Mtihani wa ngazi ya Stashahada (Diploma) watarudia Mtihani katika tarehe watakayotangaziwa, hivyo wanashauriwa kufanya maandalizi ya Mtihani huo wa Marudio na hakutokuwa na malipo yoyote kwa Watahiniwa wa Mtihani wa marudio.
- iv. Kwa wale wa Shahada na Astashahada ambao hawakufaulu watatakiwa kurudia Mtihani huo kwa utaratibu wa kawaida.
- v. Waliofaulu Mtihani wa Shahada na Astashahada watasajiliwa kwa mujibu wa utaratibu.

Niwakumbushe Watahiniwa wote **kufuata Taratibu, Kanuni za Mitihani na kuacha njia za mikato ambazo hazina tija na kuleta usumbufu usiokuwa wa lazima.**

Heri ya Mwaka Mpya na Niwatakie Maandalizi Mema.

Imetolewa Na;

AGNES MTAWA
MSAJILI

BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA